

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE

18 MEI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 18 MEI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya
Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya
Habari Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka
wa Fedha 2023/2024.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

362. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, kwa kiasi gani Vijana wa Mtwara wamenufaika na Programu ya Kukuza Ujuzi.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

363. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Shule za Sekondari Nyamtukuza, Muhange, Shuhidia, Kasanda na Gwanumpu zitakuwa za Kidato cha Tano na Sita.

364. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatangaza Mamlaka ya Mji Mdogo Bagamoyo kuwa Halmashauri.

365. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kiasi gani cha bajeti kimetengwa *TARURA* miaka mitatu mfululizo kwa ajili ya ukarabati wa barabara Kyerwa na upi ufanisi wake.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

366. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, kwa kiasi gani ushiriki wa Tanzania katika Mikutano ya Kimataifa unazingatia upatikanaji wa fursa za kiuchumi na utekelezaji wake.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

367. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali italetwa Muswada wa Sheria ya adhabu kali kwa wanaobaka na kulawiti Watoto na Wanawake.

WIZARA YA KILIMO:

368. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kwa kiasi gani Taifa linanufaika na Vijana wanaopelekwa kwenye mafunzo ya Kilimo Israel.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

369. MHESHIMIWA SHAMSIA AZIZI MTAMBA (MTWARA VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara kutoka Mtwara Mjini hadi Msimbati.

370. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini fedha za ujenzi wa barabara kutoka Makongorosi hadi Rungwa inayounganisha Mbeya, Tabora na Singida zitatolewa.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Yatokanayo na Urekebu wa Sheria wa Mwaka 2023 [*The Laws Revision (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023*].

Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa Mwaka 2023.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa Mwaka 2023 [*The Tanzania Intelligence and Security Service (Amendment) Bill, 2023*].

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA
18 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

